**JESMA 007**

# JARIBIO LA SABA K.C.P.E DARASA LA NANE 2021

**KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Chagua jibu lenye nomino zilizo katika ngeli ya I - I pekee.
A. kahawa, fedha;
B. chumvi, chupa
C. sukari, mvua
D. mali, chai

Jibu sahihi ni C

**1** [A] [B] [C] [D] **11** [A] [B] [C] [D] **21** [A] [B] [C] [D] **31** [A] [B] [C] [D] **41** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

Tovuti: www.jesmapublishers.com Barua pepe: jesmapublishers@yahoo.com

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15.** *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

Uaminifu ni __1__. Mtu __2__ mwaminifu, __3__ kuwaona waja wengine wakijitenga naye. Hii ni kwa sababu wanajua kuwa mtu huyu __4__ __5__ na kuvuruga uhusiano wao. Uaminifu ndio unaomfanya mtu kuzingatia haki __6__ daawa yoyote au hata pale ambapo __7__ ushahidi kuhusu jambo lolote __8__.

**1.** A. mambo ambayo mtu huyaamini B. hulka ya kutenda watakavyo wengine
C. hali ya kuzingatia maagizo bila kupinga D. mazoea ya kusema ukweli wakati wote

**2.** A. asipokuwa B. asiokuwa C. asiyokuwa D. asikokuwa

**3.** A. ni ajabu B. ni muhali C. ni ibra D. si ajabu

**4.** A. huja B. huenda C. pengine D. ndiye

**5.** A. akapiga debe B. akaingia kiwi C. akapika majungu D. akawaendea mbio

**6.** A. anapoamua B. anavyoamua C. anayoamua D. anayeamua

**7.** A. atoapo B. anapotoa C. anaitoa D. anautoa

**8.** A. aliyoshuhudia B. alioshuhudia C. alilolishuhudia D. aliyolishuhudia

Mwanafunzi __9__ shuleni hujifunza matumizi anuwai ya lugha. Mfano mzuri ni kutumia tashbihi kama vile __10__. __11__, mwanafunzi huyu hutumia methali __12__ ujumbe wake. Akitaka kumaanisha kuwa watu wameumbwa wakiwa na tofauti nyingi, atatumia methali '__13__'. Isitoshe, __14__ hujifunza __15__ kama vile upendo, uvumilivu na ukarimu.

**9.** A. anavyokuwa B. anaokuwa C. aliyekuwa D. anapokuwa

**10.** A. savula ni lumbwi; usimwanimi B. wanafunzi hawa wana bidii ya mchwa
C. polepole ya kobe humfikisha mbali D. mwala alituvunja mbavu kabisa

**11.** A. Ama B. Lau C. Aidha D. Japo

**12.** A. kufumbia B. kufumbua C. kufumbata D. kufumba

**13.** A. kila chombo na wimbile B. hakuna kizuri kisichokuwa na ila
C. akili ni nywele kila mtu ana zake D. mchele ni mmoja mapishi mbalimbali

**14.** A. wao B. yeye C. wewe D. ninyi

**15.** A. maadili B. maarifa C. taaluma D. stadi

*Kuanzia nambari* **16** *mpaka* **30**, *chagua jibu lifaalo zaidi.*

**16.** Tambulisha matumizi ya <u>ni</u> katika sentensi ifuatayo.
Zubedia alinipata usingizini alipofika.
A. wingi,mahali
B. nafsi, kitendo
C. nafsi, hali
D. kitenzi, mahali

**17.** Andika wingi wa sentensi hii.
Ukuni alionipa hauwaki jikoni.
A. Kuni waliyotupa haiwaki mekoni.
B. Kuni walizonipa haziwaki majikoni.
C. Kuni waliyotupa haiwaki mekoni.
D. Kuni wazizotupa haziwaki majikoni.

**18.** Chagua orodha yenye nomino za ngeli moja.
A. Wembe, umbo, wayo
B. asali, miwani, mvua
C. ulezi, wazo, mabele
D. shati, barua, shule

**19.** Ainisha maneno yaliyopigiwa vistari kwenye sentensi ifuatayo
Tulifanya kazi <u>kwa bidii</u> tukaimaliza <u>kabla ya wengine</u>.
A. kivumishi, kielezi, kihusishi
B. kihusihi, kielezi, kivumishi
C. kielezi, kihusishi, kiwakilishi.
D. kivumishi, kihusishi, kielezi

**20.** Ugonjwa wa kuvimba mashavu mpaka chini ya taya ni
A. machapwi
B. surua
C. ukoma
D. hijabu

**21.** Cheka ni kwa **mcheshi** kama vile **sahau** ni kwa
A. sahaulisha
B. sahaulika
C. kusahau
D. msahaulifu

**22.** Andika ukubwa wa sentensi hii.
Mtoto alipewa chai kwa kikombe hicho.
A. Jitoto lilipewa chai kwa jikombe hilo.
B. Toto lilipewa chai kwa kombe hilo.
C. Jitoto alipewa chai kwa jikombe hilo.
D. Kitoto kilipewa chai kwa kijikombe hicho.

**23.** Sahihisha sentensi ifuatayo
Hapa ndiko ambapo anapoishi.
A. Hapa ndiko ambako anakoishi.
B. Hapa ndipo ambapo anapoishi
C. Hapa ndipo ambapo anaishi.
D. Hapa ndipo ambapo aishipo.

**24.** Neno **sahihishiana** lina silabi ngapi?
A. sita
B. saba
C. tano
D. kumi na moja

**25.** Mashairi yapi yameainishwa kulingana na idadi ya mishororo?
A. utenzi, ngonjera
B. tathnia utenzi
C. ngonjera, tarbia
D. takhmisa, tathnia

**26.** Bainisha maelezo yaliyo sahihi
A. Ufu ni nazi iliyokunwa.
B. Kifumbu hutumia kupepetea nafaka.
C. Makombo ni chakula kilicholala.
D. Kichanja hutumiwa kuninginizia vyombo darini.

**27.** Ipi ni tofauti ya maana kati ya watatu na wa tatu
A. Watatu ni idadi ya jumla lakini wa tatu ni idadi katika orodha.
B. Watatu ni idadi kamili lakini wa tatu ni idadi ya jumla.
C. Watatu ni idadi ya makadirio lakini wa watu ni idadi kamili.
D. Watatu ni idadi kamili lakini wa tatu ni anayechukua nafasi ya tatu katika orodha.

**28.** Andika usemi halisi wa

Sela alitaka kujua iwapo tungeuimba wimbo wetu siku iliyofuata..

A. "Mnauimba wimbo wenu kesho?" Sela alituuliza

B. "Mtauimba wimbo wenu kesho?" Sela alituuliza

C. "Kesho mngeuimba wimbo wenu?" Sela aliwauliza

D. "Kesho watauimba wimbo wao?" Sela aliuliza.

**29.** Kisawe cha **staha** ni

A. ukuu

B. ndweo

C. afya

D. heshima

**30.** Chagua neno lenye sauti changamano

A. shela

B. chafua

C. andazi

D. mkufu

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kuanzia* **31** *mpaka* **40**

Watu wanaposikia kuhusu wanafunzi wenye mahitaji maalum, akili za wengi huwazia wale wasiotembea, wasioongea au pengine kusikia na kuona. Ukiwauliza ni kwa nini, huenda wakawa wepesi wa kusema kwamba wanafunzi wa aina hii hawawezi kusoma kama wengine; wanahitaji kupelekwa katika shule maalum. Jambo walisilolijua watu hawa ni kuwa, wanafunzi wa aina hii wakipewa nyenzo zinazohitajika na kuhudumiwa ipasavyo wanaweza kufanya vizuri zaidi na hata kuwapiku wale wanaotajwa kuwa wasio na kasoro.

Jambo la kusikitisha ni kuwa wanafunzi wengi wa aina hii hawapati fursa ya kutambua na kuvikuza vipawa vyao ili kujiendeleza. Wakiwa shuleni au katika jamii baadhi ya watu huwataja kwa majina kama vile kiwete, bubu, kiziwi au kipofu. Japo majina yao yanajulikana sijui ni kwa nini watu huchagua majina haya ya **kuwashushia hadhi yao**. Mwanafunzi akizoea kuitwa kwa majina haya anaweza kujiona duni kuliko wenzake. Jambo hili huenda likamwathiri kiasi cha kushindwa kufuatilia ndoto zake. Husemekana kuwa neno jiwi ni jeraha la moyo.

Mbali na wanafunzi hawa wenye uatilifu wa kimaumbile, kuna wale ambao hulka zao haziambatani na mahitaji ya shule. Wanafunzi hawa hujipata ama wakiwabugudhi walimu au wanafunzi wenzao kwa njia mbalimbali. Mara utasikia kuwa hawamalizi kazi wanazopewa, kuwapiga wenzao au labda hata hawahudhurii masomo kwa desturi. **Tukichunguza kwa kina**, tutagundua kuwa vitendo vya aina hii huwa na usuli ambao anaenda mbali hata kuliko vitendo vya darasani. Kujaribu kuwaadhibu wanafunzi wa aina hii huweza kugeuka ngoma goya.

Vituko vya aina hii huenda vinatokana na shida za nyumbani kama vile uchochole au migogoro ya wazazi. Kuna wale wanaotafuta tu kugunduliwa kwa uwepo wao kwa kuhisi kwamba wanapuuzwa na jamii au jamaa zao. Ni vyema mwalimu achunguze chanzo cha utovu wa nidhamu ili ajue njia mwafaka zaidi ya kudhibiti maadili ya mwanafunzi. Ikiwa kwa mfano upotovu huu unatokana na uraibu wa mihadarati, mwanafunzi anahitaji kutafutiwa matibabu mbali na kuusiwa ipasavyo. Ni vyema pia kuwashirikisha wazazi, wanafunzi wengine na hata idara ya ushauri nasaha. Kuvifumbia macho vitendo vya utovu wa nidhamu shuleni ni kama kupuuza kuziba ufa. Bila shaka anayefanya hivi huishia kujenga ukuta.

Kuna wanafunzi ambao huchukua muda kuelewa mambo. Ni makosa kusema kwamba wao ni wajinga. Ukweli ni kwamba wanafunzi hawa wakipewa muda wanaohitaji na kuelekezwa ipasavyo, wao hufanya vyema hata kuliko wale wanaotajwa kuwa wenye vichwa vyepesi. Ni makosa kutarajia kuwa wanafunzi hawa wakipewa mifano michache tu watamudu kutimiza malengo wanayowekewa. Njia bora zaidi ni kuwatolea mifano ya kutosha na mazoezi yatakayostawisha uelewa wao. Mwanafunzi yeyote anapopewa nafasi nzuri, huweza kuyamudu masomo yake barabara.

Kwa upande mwingine, wapo wanafunzi wenye akili nyepesi ambao kumudu masomo hakuwi mzigo kwao. Utawatambua kuwa namna wanavyodhihirisha ustadi katika kujibu maswali, kupiga hesabu na stadi nyingine zinazodhihirika darasani. Wanafunzi hawa hukamilisha mazoezi kabla ya wenzao. Juhudi za walimu za kuwafaa wengine huonekana kama kupoteza wakati kwa wanafunzi hawa. Yawezekana hata kuaona wakisinzia au kuwasumbua wenzao baada ya kukamilisha kazi zao. Wakati mwingine, kwa kutaka kudhihirisha weledi wao. Hujipata wakimdakiza mwalimu kwa maneno au kuuliza maswali mfululizo. Yafaa wahimizwe kuhusu umuhimu wa kuwapa wenzao nafasi. Aidha, waongozwe kutumia ujuzi wao kuwafaa wenzao darasani. Mwalimu anaweza kuwapa majukumu yanayowafikirisha zaidi ili wautumia ujuzi wao. Kila mmoja ana udhaifu wake. Ni vizuri tuwe wa kuvumiliana, kuheshimiana na kuthaminiana ili tukuze jamii yenye umoja.

**31.** Chagua kauli iliyo sahihi
- A. Udhaifu wa maumbile hukwamisha kabisa utendakazi wa mtu.
- B. Watu wengi hawajui huwa kuna wanafunzi wenye mahitaji maalum.
- C. Kutohudumiwa ipasavyo huwanyima wenye mahitaji nafasi ya kujiendeleza.
- D. Aghalabu wanafunzi wenye shida hawafanyi vyema shuleni.

**32.** Njia bora **ZAIDI** ya kuwafaa wanafunzi wenye mahitaji maalum shuleni ni
- A. kuwatendea yote wanayotarajia kutekelezewa.
- B. kuwapa majukumu mepesi kuliko wenzao.
- C. kuwapa nyenzo wanazohitaji na kuboresha uwezo wao.
- D. kuwatarajia kutekeleza majukumu kama ya wenzao.

**33.** Kulingana na aya ya pili
- A. kutomwita mtu jina lake ni kumvunjia heshima.
- B. kumdhalilisha mtu kimaumbile huweza kuathiri utendaji wake.
- C. watu hawapendi kutajwa kwa ulemavu wa wenzao.
- D. viwete, bubu, viziwi na vipofu hudhalilishwa zaidi shuleni.

**34.** Yote haya yametajwa kwamba huchangia kudhoofika kwa maadili **isipokuwa**
- A. hali ya uhitaji wa pale nyumbani.
- B. kutoelewana na jamaa wa familia
- C. uraibu wa dawa za kulevya
- D. wanafunzi kutomaliza kazi shuleni.

**35.** Maana ya **tukichunguza kwa kina** ni
- A. tukipeleleza kwa undani.
- B. tukizingatia kwa bidii
- C. tukichunguza kwa ujasiri
- D. tukiwazia juujuu.

**36.** Kuchunguza chanzo cha vitendo vya wanafunzi ni muhimu kwani
- A. humfanya mwalimu kuwaelewa zaidi wanafunzi wake.
- B. huwezesha kupatikana mbinu bora za kulitatua tatizo hilo.
- C. humjengea mwalimu njia bora zaidi za kusuluhisha migogoro nyumbani.
- D. huimarisha misingi ya nidhamu wanakotoka wanafunzi.

**37.** Kupuuza kuziba ufa kumelinganishwa na
- A. madhara ya kukosa kutambua matatizo ya wanafunzi
- B. madhara yanayochangia kuta kuporomoka shuleni.
- C. madhara ya kukosa kuwarekebisha wanafunzi wanaoshuhudia utovu wa nidhamu.
- D. madhara ya kupuuza upungufu wa kimaadili, miongoni mwa wanafunzi.

**38.** Katika aya ya tano, mwandishi anasema kuwa
- A. wanafunzi wanaochukua muda kuelewa mambo huwa werevu zaidi ya wenzao.
- B. Walimu wengi huwapotosha wanafunzi kwani wao hutoa mifano michache tu
- C. kupewa nafasi ifaayo humpa mtu fursa ya kutumia uwezo wake kikamilifu.
- D. wanafunzi wameanza kufanya vyema kuliko hapo awali.

**39.** Wanafunzi wenye vichwa vyepesi husaidiwa kwa
- A. kuwapa mazoezi yanayoambatana na uwezo wao.
- B. kupewa majukumu magumu darasani.
- C. kuwahimiza wenzao wawasaidie darasani.
- D. kuwaongezea muda na kuwapa mifano zaidi.

**40.** Kichwa kifaacho **ZAIDI** kwa taarifa hii ni
- A. Mifano ya walemavu katika jamii.
- B. Jinsi ya kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji maalum.
- C. Chanzo cha utovu wa nidhamu shuleni.
- D. Namna ya kuwahudumia wanafunzi wenye majitaji maalum.

*Yasome makala haya kisha ujibu maswali kuanzia* **41** *mpaka* **50**

Aushi yetu ilitumbukia nyongo baba alipoonyeshwa lango kazini. Alitueleza kwamba shirika lilianza kudidimia wasimamizi wake walipoanza kutumbukiza mikono na kuchovya kwenye buyu la kipato cha shirika hilo. Wakasahau kwamba chovyachovya humaliza buyu la asali. Walificha njama zao kwa kusawazisha hesabu kwa kalamu. Kampuni ikawa inaingia shoti siku baada ya nyingine. Awali, idadi ya wafanyakazi ilipunguzwa; waliobaki wakapunguziwa mshahara na marupurupu. Hatimaye ikajiri kwamba **mtego wa panya huingia waliokuwemo na wasiokuwemo**. Milango ya shirika ikafungwa. Baba na wenzake wakamwaga unga.

Baba alitanga huku na kule akisaka amali bila mafanikio. Kila siku, alionekana mwenye mori na kukata tamaa. Akiba yake kibindoni iliendelea kupungua kutokana na mahitaji ya nyumbani. Vitamutamu tulivyozoea vikawa havipo tena. Kwa mara ya kwanza, mimi na ndugu zangu tukaonja uchungu wa kutumwa nyumbani kuenda kuleta karo. Nakumbuka siku hiyo, wanuna wangu walilia mpaka visima vyao vya machozi vikakauka. Halikunitoka hata tone la machozi. Hapo niliumia sana moyoni sikutaka kuonyesha udhaifu machoni pa wadogo wangu hawa. Niliwaliwaza kama mzazi.

Maji yalipozidi unga, baba alituita pale sebuleni jioni moja. Alitueleza dhahiri shahiri kwamba alitaka turejee mashambani badala ya kuendelea **kula mwata** mjini. Tulilitia wazo hili kwenye mizani, tukajadiliana kwa mapana na marefu. Hatimaye tuliafikiana kuwa hili halikuwa wazo zuri tu bali pia njia ya pekee ya kukiokoa chombo chetu kabla ya kuzama kabisa. Labda wahenga walipita shida kama zetu kabla ya kunadi kuwa, 'ng'ombe alivunjika mguu malishoni hujikokota hadi zizini kusaidiwa'.

Maisha ya kijijini hayakuwa rahisi kwetu. Baba na ami zangu walishirikiana kujenga nyumba yenye vyumba vitatu iliyokandikwa kwa udongo. Kimoja, kilikuwa sebule, kingine kikawa cha wazazi huku sisi tukitumia kile cha tatu. Namkukumba kakangu mdogo akilia na kusema kuwa anataka turudi kwenye 'nyumba' kule mjini. Mama alimweleza kuwa hiyo ndiyo ilikuwa nyumba yetu. Labda ndugu huyu alishangaa nyumba itakuwaje na sakafu ya udongo bila hata nguvu za umeme.

Wavyele wangu waliinamia kazi za shamba wakakuza kila aina ya mmea. Kilimo kiliwaitikia wakavuna maridhawa msimu baada ya mwingine. Wakati huo tulikuwa tumesajiliwa katika shule ya umma iliyokuwa karibu. Jambo lililonifurahisha pale ni kwamba hapakuwa na utabaka. Huenda watoto wengi walitoka kwenye familia zilizolingana na yetu.

Nilitia fora masomoni huku nikisadiki kuwa elimu ilikuwa nguzo imara ya kuyaegemezea maisha yangu. Nilitaka kujiimarisha maishani pamoja na kufidia juhudi za wavyele wangu za kunielimisha. Walimu walinipongeza na kunituza. Wanafunzi wenzangu walinihusudu huku wazazi wakinipongeza. Ama kweli, mcheza kwao hutuzwa.

Pato kutoka shambani liliwawezesha wazazi wetu kukidhi mahitaji yetu yote. Kipaji cha baba kilinawiri tena. Alitumia mbinu bora za kilimo kujihakikishia matokeo bora zaidi. Hata nilipofaulu kujiunga na chuo kikuu, nilijua kuwa nisingekabiliwa na uhaba wa karo. Hapo nikaamua kuwa wembe ungekuwa ule ule. Tangu wakati huo, katu sijatazama nyuma wala kusitisha juhudi zangu.

**41.** Katika aya ya **kwanza** msimulizi anasema kuwa; baba
A. yake alifutwa kazi kwa kushiriki ufisadi.
B. yake alikuwa msimamizi alikofanyia kazi.
C. alifutwa kazi kutokana na kupunja shirika lake.
D. aliathirika baada ya kampuni kufilisika.

**42.** Inaonekana wazi kuwa
A. familia haikuwa na chochote baba alipoachishwa kazi.
B. awali, familia iliendelea kujikimu hata baada ya baba kuachiswa kazi.
C. kuachishwa kazi kulimfanya baba apoteze matumaini
D. kutiliwa fitina ndiko kulikomfanya baba afutwe kazi.

**43.** Methali, **'mtego wa panya huingia waliokuwemo na wasiokuwemo'** inadhihirika kwa kuwa
A. njama za ufisadi ziliwafanya hata waliohusika wakamwaga unga.
B. kufutwa kazi kwa baba kulisababisha familia nzima kuathirika.
C. wizi mdogomdogo ulisababisha shirika zima kuporomoka.
D. kufungwa kwa kampuni kulifanya wengi kuhamia mashambani.

**44.** Msimulizi hakulia kama wadogo wake kwa sababu
A. alikuwa amezoea tabu; kinyume na wenzake
B. hakuhisi uchungu kama waliohisi ndugu zake.
C. hakutaka kupoteza hadhi yake.
D. alikuwa kama mzazi kwa wenzake.

**45.** Baba ni mlezi bora anayepaswa kuigwa. Hii ni kwa sababu
A. alihusisha jamii nzima katika maamuzi.
B. aliamua kuhamishia familia mashambani ili kuepuka shida.
C. aliwaita wote na kuwaagiza kumfuata mashambani.
D. hakukata tamaa licha ya shida nyingi.

**46.** Kilio cha kaka mdogo kinaonyesha kuwa,
A. watu wa mjini walikuwa wazuri kuliko wa mashambani.
B. nyumba ya mjini ilikuwa na vyumba vingi kuliko ya mashambani.
C. Maisha ya mashambani yalikuwa mabaya kwa kukosa makazi.
D. nyumba ya mjini ilikuwa bora kuliko ya mashambani.

**47.** Maisha katika shule ya umma yalikuwa bora kwa msimulizi kwani,
A. wanafunzi wote walitoka katika jamaa maskini.
B. wanafunzi hawakubaguana kwa misingi ya kiuchumi.
C. hali yake ilikuwa bora kiasi ikilinganishwa na wenzake.
D. shule hii ilikuwa na nafasi kuliko ya mjini.

**48.** Juhudi za msimulizi katika shule mpya zilitokana na
A. nia ya kuwasaidia wazazi waliopitia shida nyingi.
B. kulipia jitihada walizofanya wazazi wake.
C. tuzo mbalimbali alizopewa na walimu wake.
D. haja ya kudhihirisha umahiri kwa wenzake shuleni.

**49.** Msemo **kula mwata** jinsi ulivyotumika una maana sawa na,
A. kula mumbi
B. kula mwande
C. kwenda nguu
D. kusalimu amri

**50.** Kulingana na aya ya mwisho,
A. kujiunga na chuo kikuu kulimfanya msimulizi kuthamini bidii.
B. kufanikiwa kwa msimulizi kulimfanya baba anawiri kipaji.
C. kutumia mbinu zifaazo humhakikishia mtu matokeo bora zaidi.
D. mafanikio yalimfanya msimulizi kusahau aliyopitia maishani.